

KIWANGO GHA MSINGI



1 somo 1

Njaa ni Nini na Wenye Njaa ni Nani?

Jumla ya muda wa somo: dakika 45



Lengo 1

Kuelewa kwa nini tunahitaji chakula

Dhana

- Sote tunahitaji chakula
- Chakula hutupa nguvu na virutubishi tunavyohitaji ili kuifanya miili yetu kuendelea kufanya kazi, kukua na kustawi, kutembea, kucheza, kufikiri na kusoma
- Chakula kidogo au kingi mno siyo kizuri kwa afya



Lengo 2

Kujua kuwa tunahitaji aina nyingi tofauti ya vyakula

Dhana

- Watu wanahitaji aina nyingi tofauti ya vyakula ili kuwa na afya na kukua



Lengo 3

Kujua ni nani mwenye njaa ulimwenguni

Dhana

- Njaa ni kutopata kiasi cha kutosha cha vyakula mwafaka kukidhi mahitaji yetu
- Nchi zote na maeneo yote yana baadhi ya watu wenye njaa

2

somo 2

Kwa nini Watu wana Njaa?

Jumla ya muda wa somo: dakika 45



Lengo 1

Kuelewa mfumo wa chakula unaowalisha watu

Dhana

- Mfumo unaotupa chakula unahusisha hatua nyingi



Lengo 2

Kuelewa maana ya kuwa na uhakika wa chakula

Dhana

- Kuwa na uthabiti wa chakula ina maana kwamba ni lazima kila wakati tuweze kupata chakula tunachohitaji kwa maisha biabia na yenye afya
- Nguzo tatu za uthabiti wa chakula ni: kupatikana, kufikika na utumiaji wa chakula

3

somo 3

Tunaweza Kufanya Nini ili Kusaidia Kumaliza Njaa

Jumla ya muda wa somo: dakika 45



Lengo 1

Kujua kuwa sote tunaweza na lazima tufanye jambo fulani ili kupambana na njaa

Dhana

- Kili mtu anaweza kuwa shujaa kwa kupambana na njaa



Lengo 2

Kutambua jinsi ambavyo tunaweza kupambana na njaa katika jamii zetu

Dhana

- Tunaweza kutenda jambo fulani ili kusaidia kumaliza njaa

